SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 22 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) DESEMBA 2022

MENEJIMENTI, MAAFISA BAJETI TSC WANOLEWA

Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Mectildis Kapinga akitoa mada ya uelewa kuhusu Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakati wa mafunzo ya Mipango na Bajeti yaliyowahusisha Wajumbe wa Menejimenti na Maafisa Bajeti wa TSC yaliyofanyika Oktoba 27, 2022 jijini Dodoma.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania

HONGERENI WALIMU KWA KAZI KUBWA MLIYOIFANYA MWAKA 2022

Mwaka unapoanza ni wazi kuwa watu wanajiwekea malengo ya kile wanachotamani kukifanya kwa mwaka mzima. Malengo yanatupa dira ya wapi tunapotaka kufika na kupitia malengo hayo tunaweza kujipima kama tunapiga hatua ya mafanikio au la.

Hali kadhalika kwa upande wa walimu, mwanzoni mwa mwaka tuliweka malengo ya namna ya kutekeleleza majukumu yetu kwa mujibu wa taratibu na dhumuni kubwa ni kuhakikisha mwanafunzi anapata ujuzi na maarifa kama ilivyokusudiwa.

Ni wazi kuwa katika safari ya mwaka mzima, walimu wamefanya kazi kwa bidii, weledi na uzalendo huku wakizingatia miiko na maadili ya kazi yao kitu ambacho kimesababisha kiwango cha ufaulu wa wanafunzi kuendelea kuongezeka. Hata hivyo, tunatambau kwamba wapo walimu wachache ambao bado wanafanya kazi kwa mazoea, wengine wakiendeleza vitendo vya utovu wa nidhamu kitu ambacho kinarudisha nyuma maendeleo ya elimu nchini.

Tunapokaribia kumaliza mwaka, ni wakati wa kila mmoja kufanya tathmini ya kile alichokitekeleza ili kuona ni wapi alifanikiwa na wapi alishindwa kupata mafanikio ili tuanapouanza mwaka 2023 vile vikwazo vilivyojitokeza mwaka 2022 visijirudie.

Tunawapongeza walimu kwa kufanya kazi nzuri ya kutoa huduma ya kufundisha wanafunzi na tunawatakia kila lililojema katika kuumaliza mwaka 2022. Pia, tunatarajiwa mwaka 2023 utakuwa na mafanikio zaidi katika kuwahudumia wanafunzi. Kwa wale ambao hawakutimiza majukumu yao vizuri kwa mwaka 2022, ni vyema wakajitafakari ili wanapoingia mwaka 2023 waweze kubadili tabia zao na kuona umuhimu wa kuwapa wanafunzi haki yao ya kupata elimu bora.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imejipanga vizuri katika kuhakikisha inaendelea kutoa huduma bora kwa walimu kwa mujibu wa sharia kanuni na taratibu ikiwa ni pamoja shughulikia masuala ya ajira, maadili na maendeleo ya walimu kwa ajili ya ustawi wao.

BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti
Paulina Nkwama

Wajumbe
Richard Odongo
Revocatus Misonge
Mectildis Kapinga
Lameck Mbeya
Zachary A. Dida

Mhariri Mkuu
Gerard Chami

Mhariri
Adili Mhina

Msanifu Kurasa
Lucas Gordon

KATUNI

OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI
WA WALIMU (TSC)

HONGERA

Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Kwa kutunukiwa Shahada ya Juu ya Heshima ya Udaktari wa Falsafa ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

MENEJIMENTI, MAAFISA BAJETI TSC WANOLEWA

Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Mectildis Kapinga akitoa mada ya uelewa kuhusu Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakati wa mafunzo ya Mipango na Bajeti yaliyowahusisha Wajumbe wa Menejimenti na Maafisa Bajeti wa TSC yaliyofanyika Oktoba 27, 2022 jijini Dodoma.

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeendesha mafunzo kwa Wajumbe wa Manejimenti na Maafisa Bajeti wa Tume hiyo kuhusu Mpango na Bajeti kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa bajeti ya TSC ya mwaka 2022/2023 na maandalizi ya mpango na bajeti kwa mwaka 2023/2024.

Mafunzo hayo yaliyofanyika kwa siku tatu kuazia Novemba 15 – 17, 2022 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kiwete (JICC) jijini Dodoma na yaliendeshwa na Afisa anayeshughulikia masuala ya uchumi kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Samson Mangasin yaliwahusisha Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo na Afisa mmoja kutoka kila Idara na Kitengo ambao wamepewa jukumu la kushughulikia bajeti katika maeneo yao.

Wakati wa kuanza kwa mafunzo hayo, Mkurugenzi Msaidizi wa Aijira na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Mecktildis Kapinga aliwasilisha mada iliyohusu majukumu na muundo wa TSC hiyo ambapo alisema kuwa Tume hiyo iliundwa kwa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015 na ilianza kutekeleza majukumu mwaka 2016 na kuongeza kuwa lengo la kuanzishwa kwake ni kutoa huduma bora za kiutumishi kwa Walimu wa Serikali wanaofundisha shule za Msingi na Sekondari.

Mchumi Mkuu kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ambaye pia ni Mkufunzi wa Mafunzo ya Mipango na Bajeti, Samson Mangasin akitoa mada wakati wa mafunzo hayo yaliyowahusisha Wajumbe wa Menejimenti na Maafisa wa TSC. Mafunzo hayo yalifanyika Novemba 15 – 16, 2022 jijini Dodoma.

MENEJIMENTI, MAAFISA BAJETI TSC WANOLEWA

Kwa upande wa masuala ya mipango na bajeti, washiriki walipitishwa katika mada mbalimbali zikiwemo utaratibu wa uandaaji na utekelezaji wa bajeti, Mwongozo wa Mpango na Bajeti, Mpango Mkakati, Uandaaji wa Malengo na Shabaha, Uwasilishaji wa Bajeti na Ufuatiliaji pamoja na Taarifa za Utekelezeji wa bajeti husika.

Mwezeshaji alieleza kuwa uandaaji na utekelezaji wa bajeti unazingatia mambo mbalimbali ikiwemo Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015, Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001, Sheria ya Mwaka ya Fedha (Annual Finance Act), Dira ya

Washiriki wa Mafunzo ya Mipango na Bajeti wakiendelea kufuatilia mada inayowasilishwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Mectildis Kapinga wakati wa mafunzo hayo.

Washiriki wa Mafunzo ya Mipango na Bajeti wakiendelea kufuatilia mada inayowasilishwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Mectildis Kapinga wakati wa mafunzo hayo.

MENEJIMENTI, MAAFISA BAJETI TSC WANOLEWA

Maendeleo ya Taifa 2025, Mpango wa Taifa wa Maendeleo (National Development Plan) pamoja na Mwongozo wa Mpango na Bajeti (Plan and Budget Guideline (PBG)).

Pia, alieleza kuwa bajeti ya Serikali inapaswa kusaidi wananchi kuwa na maisha bora (High quality livelihood), kuwa na uchumi imara (Strong and competitive economy), kuwa na Utawala bora (Good governance), kuwa na Taifa lenye watu walioelimika (A well educates and learning population), pamoja na kuchochea Amani, Umoja na Mshikamano (Peace, stability and unity).

Kuhusu Mwongozo wa Mpango na Bajeti, mwezeshaji aliwaeleza washiriki namna ya kuanda bajeti kwa kuzingatia miongozo inayotolewa na Wizara ya Fedha, pia alieleza kuwa ukomo wa bajeti unategemea makusanyo na rasilimali zilizopo.

Aidha, mwezeshaji alitoa wasilisho kuhusu uandaaji wa Malengo na shabaha janja (Smart Objective, Target & Activity) ambapo alieleza kuwa uandaanji mzuri wa malengo na shabaha husaidia utekelezaji mzuri wa majukumu kwani huleta ufanisi endapo kutatokea uhaba wa rasilimali hivyo kuwezesha kutoa kipaumbele kwa shabaha na kazi muhimu zaidi kwa Taasisi.

Mwezeshaji alifundisha na kuelezea juu ya Uwasilishaji wa Bajeti (Budget Presentation) na Ufuatiliaji pamoja na Taarifa za Utekelezeji ambapo alieleza kuwa taarifa za Robo mwaka zinapaswa kukusanywa ndani ya siku 30 baada ya kuisha kwa robo husika huku akisisitiza kuwa taarifa ya utekelezaji wa mwaka inapaswa kukusanywa kabla au inapofika tarehe 15 October baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha.

Nao washiriki wa mafunzo hayo ambao walipata fursa ya kuuliza maswali na kupatiwa majibu walikiri kuongeza uelewa wa masuala mbalimbali ya uandaaji na utekelezaji wa bajeti na hivyo kusaidia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya chombo hicho cha kuhudumia walimu katika masuala ya kiutumishi.

Washiriki wa Mafunzo ya Mipango na Bajeti wakiendelea kufuatilia mada zilizokuwa zinawasilishwa katika mafunzo hayo.

Kikao cha ufuatiliaji wa majukumu ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi ya Wilaya kikiwa kinaendelea katika ofisi ya TSC Wilaya ya Mbinga.

Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Mbinga, Grace Mbena (kulia) akitoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo kwa maafisa kutoka TSC Makao Makuu (hawapo pichani) waliofika ofisini hapo kwa lengo la kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo.

OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI
WA WALIMU (TSC)

SIKU YA UKIMWI DUNIANI

01, DISEMBA 2022

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) inaungana na Watanzania wote na Dunia nzima kuadhimisha Siku ya UKIMWI Duniani.

www.tsc.go.tz

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania

Walimu wana uelewa mkubwa wa taratibu za utumishi: TSC Namtumbo

Na Mwandishi wetu - Namtumbo.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Namtumbo imeeleza kuwa walimu inaowahudumia wamekuwa na uelewa mkubwa wa sheria kanuni na taratibu za utumishi wa walimu kitu ambacho kimepunguza ukiukwaji wa taratibu za kiutumishi kwa walimu wa wilaya hiyo.

Hayo yamebainishwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Namtumbo, Abel Nyoni wakati alipokutana na timu ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo kutoka TSC Makao Makuu iliyofika ofisini hapo hivi karibuni ambapo alieleza kuwa ofisi hiyo inahudumia jumla ya walimu 1273 ambapo walimu 867 ni wa shule za msingi na 406 ni wa sekondari.

"Walimu wameedelea kuimarika katika kuielewa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2016 na Kanuni za Utumishi wa Umma. Viashiria vya uelewa huo tunaviona kwa kuangalia idadi ndogo ya mashauri ya nidhamu tunayoyashughulikia kwa mwaka," alisema Nyoni.

Alifafanua kuwa katika kipindi cha miaka mitatu jumla ya mashauri 11 yalifunguliwa ambapo utoro uliongoza ukiwa na mashauri manne (4) ikifuatiwa na makosa ya rushwa yaliyokuwa na mashauri mawili huku adhabu mbalimbali zikitolewa ikiwemo

Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Namtumbo, Abel Nyoni akitoa ufafanuzi juu ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo wakati timu ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu wa ofisi za TSC ngazi ya wilaya ilipowasili ofisini hapo hivi karibuni.

Afisa wa TSC Wilaya ya Namtumbo anayeshughulikia Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu akiwa ofisini kwake.

Walimu wana uelewa mkubwa wa taratibu za utumishi: TSC Namtumbo

Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu wa TSC Makao Makuu, Ramadhan Ngaegela akizungumza na watumishi wa TSC Wilaya ya Namtumbo (hawapo pichani) katika ofisi za TSC Namtumbo hivi karibuni.

kufukuzwa kazi, karipio na onyo na walimu wengine waliachiwa huru kwa kuwa hawakupatikana na hatia.

"Mwaka 2020/2021 kulikuwa na mashauri matano (5) ambayo yalihusu uhusiano wa kimapenzi wa mwalimu na mke wa mtu (1), kukaidi amri (1), utoro (1) na wizi wa mitihani (1). Mwaka 2021/2022 kulikuwa na mashauri mawili (2) ambayo yalihusu utoro na uzembe," alisema.

Aliongeza kuwa, "mwaka 2019/2020 kulikuwa na mashauri matano (5) ya nidhamu ambapo mashauri hayo yalihusu rushwa (2), utoro kazini (2) na uchonganishi mahali pa kazi (1)."

Akiongelea kuhusu Ajira na Maendeleo ya Walimu, alisema kuwa jumla ya walimu 54 waliajiriwa ambapo katika idadi hiyo walimu 24 walikuwa ni wa shule za msingi na walimu 30 walikuwa ni wa shule za sekondari.

"Katika mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya walimu 91 walipandishwa vyeo ambapo walimu 53 walikuwa wa shule za msingi na walimu 38 walikuwa wa shule za sekondari," alisema.

Pamoja na mafanikio hayo, Kaimu Katibu Msaidizi huyo alieleza kuwa ofisi yake inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo upungufu wa vyumba vya ofisi, upungufu wa watumishi, kutokuwa na chombo cha usafiri kwa ajili ya kuwafikia walimu mara kwa mara pamoja na kutokuwa na miundombinu ya mtandao wa intaneti.

Kiongozi huyo alihitimisha kwa kuomba Tume Makao Makuu kuona namna inavyoweza kuiwezesha ofisi hiyo ili utekeleze majukumu yake kwa ufanisi Zaidi.

Wilaya ya Namtumbo ina jumla ya shule 136; kati ya hizo shule 111 ni za msingi na shule 25 ni za sekondari.

Piacha ya Pamoja kati ya watumishi wa TSC Wilaya ya Namtumbo na Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu wa TSC Makao Makuu, Ramadhan Ngaegela (katikati).

WALIMU 45 SONGEA WAENDA MASOMONI

Na Mwandishi wetu – Songea.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Songea imesema kuwa walimu 45 kutoka shule za msingi na sekondari za serikali katika Halimashauri ya Manispaa ya Songea, Halmashauri ya Wilaya ya Songea pamoja na Halmashauri ya Madaba wapo masomoni.

Kauli hiyo imetolewa na Afisa anayeshughulikia Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu wilayani hapo, Mathew Komba kwa niaba ya Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Songea wakati akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo kwa timu ya ufuatiliaji kutoka TSC Makao Makuu iliyotembelea ofisi hiyo kwa lengo la kupata taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Komba alisema kuwa Tume hiyo imeendelea kutoa elimu kwa walimu juu ya umuhimu wa kujiendeleza kimasomo kwani inawawezesha kutoka hatua moja kwenda nyingine kiutumishi na kueleza kuwa walimu wameendelea kuwa na mwitikio chanya katika kujiendeleza.

"Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Songea inahudumia jumla ya Halmashauri tatu ambazo ni Manispaa ya Songea, Songea DC na Madaba DC. Katika suala la kujiendeleza kielimu walimu wetu wana mwitikio mzuri, kwa mfano kwa sasa jumla ya walimu 45 wapo masomoni. Katika idadi hiyo walimu 36 ni kutoka Manispaa ya Songea, walimu sita (6) ni kutoka Halmashuri ya Wilaya Songea na Walimu watano (5) wanatoka Halmashauri ya Madaba," alisema.

Kikao kati ya watumishi wa TSC Songea na Maafisa wa TSC Makao Makuu waliofika ofisini hapo kwa lengo la kufanya ufuatiliaji utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo hivi karibuni kikiwa kinaendelea.

Aliendelea kueleza kuwa walimu wanahamasika kwenda masomoni hasa pale wanapoona wenzao waliokwenda masomoni na kuhitimu masomo yao wanapata faida ya kubadilishwa

Afisa wa TSC Wilaya ya Songea, Mathew Komba akitoa ufafanuzi wa utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo kwa timu ya ufuatiliaji wa majukumu ya ofizi za TSC ngazi ya Wilaya (hawapo pichani) kwa niaba ya Kaimu Katibu Msaidizi wa ofisi hiyo.

WALIMU 45 SONGEA WAENDA MASOMONI

kutoka cheo cha daraja la chini kwenda cheo cha daraja la juu huku akieleza kuwa katika mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya walimu 36 walibadilishiwa kazi/cheo baada ya kujiendeleza.

Pamoja na kuwahimiza walimu kujiendeleza kielimu, alifafanua kuwa utaratibu unazingatiwa ikiwa ni pamoja na kusimamia mpango wa mafunzo ili kuhakikisha kuwa walimu wengi hawatoki kweye kituo cha kazi kwa wakati mmoja kitu ambacho kinaweza kuathiri ufundishaji wa wanafunzi shuleni.

Akizungumzia kuhusu maju-kumu mengine yanayotekelezwa na ofisi hiyo Komba alisema Wilaya ya Songea ilipawatia usajili walimu 63 wa ajira mpya ambapo katika idadi hiyo walimu 37 ni wa shule za Sekondari za Halmashauri ya Manispaa ya Songea, walimu 20 ni wa Shule za Msingi na 20 wa sekondari kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Songea pamoja na walimu wawili (2) wa shule za msingi na wengine sita (6) wa shule za sekondari za Halmashauri ya Madaba.

"Zoezi la upandishwaji vyeo Wilaya ya Songea lilifanyika vizuri na jumla ya walimu wa 351 wa shule za msingi na 175 wa sekondari walipandishwa ambapo Halmashauri ya Manispaa ya Songea walimu 295 msingi na 123 Sekondari walipandishwa. Hamlashauri ya Wilaya ya Songea walimu 50 msingi na 32 sekondari walipandishwa huku Halmashauri ya Madaba wakipandishwa walimu sita (6) wa shule za msingi na 20 wa shule za sekondari," alisema.

Picha ya pamoja kati ya watumishi wa TSC Wilaya ya Songea na Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu wa TSC Makao Makuu, Ramadhan Ngaegela (wa pili kutoka kulia).

Kwa upande wa nidhamu kwa walimu, Komba alieleza kuwa hali ni nzuri kwani walimu wameendelea kumarika katika kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za utumishi wa walimu kitu ambacho kimefanya mashahuri ya nidhamu kuendelea kupungua ambapo alibainisha kuwa mwaka wa fedha 2019/2020 kulikuwa na mashauri 17, mwaka 2020/2021 mashauri 14 na mwaka 2021/2022 kulikuwa na mashauri saba (7).

TSC Songea inahudumia jumla ya shule za msingi 187 na sekondari 49 kutoka Halmashauri zote tatu ambapo Halmashauri ya Manispaa ya Songea ina shule za msingi 81 na sekondari 24, Halmashauri ya Wilaya ya Songea shule 78 msingi na 17 sekondari huku Halmashauri ya Madaba ikiwa na shule 28 za msingi na nane (8) za sekondari.

Aidha, TSC Songea inahudumia jumla ya walimu wa msingi 1890 na sekondari 1207 kutoka Halmashauri zote tatu ambapo Halmashauri ya Manispaa ya Songea ina walimu 1200 wa shule za msingi na walimu 784 wa sekondari, Halmashauri ya Wilaya ya Songea ina walimu 497 wa shule za msingi na wa walimu 284 wa shule za sekondari huku Halmashauri ya Madaba ikiwa na walimu 193 wa shule za msingi na 139 wa shule za sekondari.

WALIMU 120 WAPANDISHWA VYEO TUNDURU

Na Mwandishi wetu – Tunduru.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Tunduru imepandisha vyeo walimu 120 wa shule za msingi na sekondari katika kipindi cha mwaka 2021/2022 ikiwa ni sehemu ya jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita katika kuboresha sekta ya elimu na walimu nchini.

Hayo yamebainishwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Tunduru, Julius Nchimbi wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi yake kwa timu ya ufuatiliaji kutoka TSC Makao Makuu iliyofanya ziara katika ofisi hiyo hivi karibuni.

Nchimbi alieleza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa mstari wa mbele hasa katika kushughulikia maslahi ya walimu kitu ambacho kimesaidia kumaliza malalamiko ya walimu hususan katika eneo la upandishwaji vyeo.

Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Tunduru, Julius Nchimbi akitoa ufafanuzi wa utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo kwa timu ya ufuatiliaji wa majukumu ya ofizi za TSC ngazi ya Wilaya (hawapo pichani) kwa niaba ya Kaimu Katibu Msaidizi wa ofisi hiyo.

"Toka Rais Samia Suluhu Hassan aingie madarakani walimu wanapata maslahi yao kwa wakati na sasa hakuna malalamiko tena. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya walimu 120 wamepangishwa vyeo, ambapo 91 ni wa shule za msingi na 29 wa sekondari. Zoezi la upandishaji vyeo lilifanyika kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizotolewa," alisema Nchimbi.

Kikao kati ya watumishi wa TSC Tunduru na Maafisa wa TSC Makao Makuu waliofika ofisini hapo kwa lengo la kufanya ufuatiliaji utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo hivi karibuni kikiwa kinaendelea.

Nchimbi alisema kuwa majukumu mengine yanayotekelezwa na ofisi yake ni pamoja na kushughulikiwa ukamilishaji wa ajira za walimu wapya kazini,kuthibitisha kazini walimu, kuwabadilishia cheo walimu waliojiendeleza kielimu, kutoa vibali vya kustaafu kazi ya ualimu, pamoja na kushughulikia maadili na nidhamu ya walimu.

"Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2022/2023

WALIMU 120 WAPANDISHWA VYEO TUNDURU

Picha ya pamoja kati ya watumishi wa TSC Wilaya ya Tunduru na Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu wa TSC Makao Makuu, Ramadhan Ngaegela (wa pili kutoka kulia).

Wilaya imeshirikiana na Mkurugenzi kujazisha mikataba ya kudumu walimu 85 ambapo walimu hao walipatiwa namba za usajili (TSC namba), walimu hao pia waliandikiwa barua za ajira," alisema Nchimbi.

Akizungumzia kuhusu kuthibitisha kazi walimu, Kaimu Katibu Msaidizi huyo alieleza kwamba walimu wanapoingia kwenye ajira wanapewa muda wa matazamio ili kuona kama wanafaa kuwa watumishi wa Umma ambapo alieleza kuwa kipindi hicho ni cha kati ya miezi nane (8) hadi miezi 12 na ikiwa kuna ambaye ataonekana hajakidhi vigezo ataongezewa kipindi cha matazamio cha miezi sita (6).

"Kwa mwaka huu wa fedha 2022/2023 tayari tumefanikiwa kuthibitisha kazini walimu 102 wakiwepo walimu 70 wa shule za msingi na walimu 32 wa shule za sekondari. Mwalimu mmoja (1) wa Sekondari ameongezewa muda wa miezi sita kutokana na kutokidhi vigezo vya kuthibitishwa kazini," alisema.

Akizungumzia kuhusu nidhamu, Nchimbi alisema kuwa hali ya nidhamu ya walimu ni nzuri huku akieleza kuwa katika kipindi cha miaka mitatu mashauri 21 yalifunguliwa huku kosa la udanganyifu wa mitihani likiongoza kwa kuwa na mashauri 12 kati ya 21.

Katika mwaka wa fedha 2019/2020 kulikuwa na mashauri 15, mwaka 2020/2021 mashauri matatu (3), mwaka 2021/2022 kulikuwa na mashauri matatu (3). Katika Mashauri hayo, makosa 12 yalihusu udanganyifu wa mitihani na hii ilitokea katika mwaka wa fedha 2019/2020, makosa ya utoro kazini yalikuwa matano (5), kukataa uhamisho makosa mawili (2) na makosa ya ulevi wakati wa kazi yalikuwa mawili (2)," alisema.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Tunduru ina jumla ya shule za serikali 152 za Msingi, 26 za sekondari na shule shikizi ni 13. Wilaya hiyo ina jumla ya walimu 1571 ambapo walimu 1142 ni wa shule za msingi na 429 ni wa shule za sekondari.

RAIS SAMIA ANATHAMINI MCHANGO WA WALIMU KATIKA SEKTA YA ELIMU - BASHUNGWA

Na. Mwandishi Wetu – Karagwe – Kagera.

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Mbunge wa Jimbo la Karagwe, Mhe. Innocent Bashungwa amesema kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan anathamini mchango wa Walimu katika kuendeleza Sekta ya Elimu nchini.

Ameyasema hayo leo tarehe 18 DESEMBA 2022 wakati akifungua Mkutano wa Umoja wa Walimu Wakuu wa shule za msingi ndani ya wilaya ya Karagwe (TAPSHA), Mkoani Kagera.

"Kwa muda ambao nimehudumu katika maeneo mbalimbali kumsaidia Mheshimiwa Rais Samia, nimeona anavyothamini Mchango wa Walimu katika kuendeleza sekta ya elimu nchini" Amesema Waziri Bashungwa.

Waziri Bashungwa amesema Serikali inaendelea kuweka Mazingira wezeshi ya ujifunzaji kwa wanafunzi na ufundishaji kwa Walimu ikiwa ni pamoja na kuangazia mahaitaji ya Walimu na miundombinu katika vituo vyao vya kazi.

Amesema katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23, Mheshiwa Rais ameiwezesha Serikali kutenga fedha za kujenga nyumba za Walimu kwa kuanzia katika maeneo ambayo miundombinu sio rafiki kijografia ambapo utaratibu huo utaendelea kila mwaka.

Aidha, Waziri Bashungwa amewahakikishiwa Walimu hao, kuwa atafikisha risala na maombi yao kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mhe. Angellah Kairuki ambayo yanaelezea umuhimu na dhamira ya kuendeleza Umoja wao wa TAPSHA ambapo yeye ndiye Mlezi wao.

Vile vile, Bashungwa amemshukuru Rais Samia kwa kuendelea kupeleka fedha nyingi za miradi ya maendeleo katika wilaya Karagwe, ikiwa ni pamoja na Ujenzi wa Shule na nyumba vya madarasa, Mradi wa maji rwakajunju , Ujenzi na ukarabati wa Barabara, pia Miradi katika sekta ya Afya.

WALIMU NA WANAFUNZI 132 WA TANZANIA WAPATA "TUZO YA BALOZI WA CHINA"

Na. Tovuti ya Gazeti la Umma – Novemba 14, 2022

Jumla ya Walimu na Wanafunzi 132 wameripotiwa kupata tuzo ya Ubalozi wa China nchini Tanzania hivi karibuni ambapo Walimu na Wanafunzi hao wametoka katika Vyuo Vikuu vinne na Shule za Sekondari tisa.

Taarifa ya kutolewa kwa Tuzo hiyo imetolewa na Tovuti ya Gazeti la Umma nchini China ikirejea kufanyika kwa hafla hiyo ya tano tarehe 10 Novemba, 2022 ambapo "Tuzo ya Balozi wa China" ilitolewa kwa Walimu na wanafunzi tajwa.

Akizungumza katika hafla hiyo Balozi wa China nchini Tanzania, Chen Mingjian, aliwapongeza Walimu na Wanafunzi hao waliopata tuzo hiyo akitumaini kuwa Vijana na Walimu hao wa lugha ya Kichina wa Tanzania watapata mafanikio makubwa zaidi katika masomo na mafunzo ya lugha ya Kichina, na kuongeza urafiki kati ya Taifa la China na Tanzania.

Mkutano wa Umoja wa Walimu Wakuu wa shule za msingi ndani ya wilaya ya Karagwe (TAPSHA), Mkoani Kagera.

TIMU YA UFUATILIAJI YABAINISHA HALI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TSC WILAYANI SIMANJIRO

Na Mwandishi Wetu – Simanjiro.

Wilaya ya Simanjiro ni miongoni mwa wilaya zinazounda Mkoa wa Manyara. Wilaya ina eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 20,591, kwa upande wa kusini Simanjiro inapakana na Wilaya ya Kondoa, Kiteto na Handeni, upande wa Mashariki inapakana na Korogwe, Same na Mwanga, upande wa kaskazini Moshi vijijini, Hai na Arumeru na kwa magharibi inapakana na Monduli na Babati.

Wilaya hiyo ina shule za msingi za Serikali 84 na 18 za binafsi zenye jumla ya wanafunzi 41,041 (wavulana 21789 na wasichana 19,252) ambapo shule hizi zinafundishwa na jumla ya walimu 620 na kwa upande wa sekondari, kuna shule 16 za Serikali zenye walimu 277.

Hayo yamebainishwa kweye taarifa ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi ya wilaya uliofanyika hivi karibuni katika ofisi mbalimbali za Tume hiyo.

Taarifa hiyo imebainisha kuwa mwaka wa fedha 2021/2022 TSC Wilaya ya Simanjiro iliwasajili walimu 40 walioajiriwa na serikali ambapo walimu wa shule za Msingi walikuwa 24 na walimu wa Sekondari 16 na huku mwaka 2022/2023 iiwa imewasajili walimu 35 wakiwemo walimu 25 wa shule za msingi na 10 wa shule za sekondari.

Iliendelea kueleza kuwa, jumla ya walimu 40 walithibitishwa kazini kwa mwaka 2022 ambapo Walimu wa msingi ni 24 na walimu wa Sekondari ni 16 na kufafanua kuwa hakuna mwalimu ambaye hajathibitishwa kazini kwa sababu mbalimbali.

Taarifa hiyo iliendelea kufafanua kuwa suala la kupandisha vyeo walimu linazingati mambo mbalimbali yakiwemo; uwepo wa ikama na bajeti iliyoidhinishwa, taarifa ya utendaji kazi wa mtumishi (OPRAS), muundo pamoja na maelekezo na miongozo mbalimbali inayotolewa na Serikali.

"Idadi ya walimu waliopandishwa cheo katika Wilaya ya Simanjiro kwa mwaka 2021/2022 ni 20, kati ya hao walimu nane (8) ni wa shule za Msingi na walimu 12 ni wa shule za Sekondari. Walimu wote waliopandishwa walibadilishiwa mishahara yao kwa wakati. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 TSC Simanjiro inatarajia kupandisha cheo walimu 226 wakiwemo 178 wa Msingi na 48 Sekondari. Sambamba na upandishwaji vyeo walimu, jumla ya walimu 17 walibadilishiwa cheo, walimu nane (8) wakiwa ni wa shule za msingi na walimu tisa (9) wa shule za sekondari," taarifa hiyo ilisema.

Kuhusu walimu kwenda masomoni, taarifa hiyo ilisema mpango wa mafunzo kwa walimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro upo, na walimu 31 wapo masomoni. Taarifa hiyo ilifafanua pia kwa waka wa fedha 2021/2022 vibali vine vya kustaafu kazi ya ualimu vilitolewa ambapo walimu wawili (2) walistaafu kwa lazima na wengine wawili (2) walistaafu kwa hiari.

"Katika mwaka 2021/2022 Shauri moja lilipokelewa na kuhitimishwa. Mwaka 2022/2023 mashauri matatu yamepokelewa na yanaendelea kushughulikiwa," ilisema taarifa hiyo.

Pamoja na hayo, katika mwaka 2021/2022 jumla ya shule 22 zilitembelewa kwa lengo la kutoa elimu kwa walimu juu ya masuala mbalimbali ya kiutumishi ambapo jumla ya walimu 113 walifikiwa.

MAREKEBISHO YA MTAALA YAZINGATIE ELIMU YA KODI – MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA YAPENDEKEZA

Na Mwandishi Wetu – Dodoma.

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) tarehe 25/09/2022 walikutana na kamati ya Kitaifa ya uboreshaji wa Mitaala inayoongozwa na Prof.Makenya Maboko jijini Dodoma kwa lengo la kutoa maoni na mapendekezo kuhusu uboreshaji wa Mitaala unaondelea.

Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipa Kodi kutoka Mamlaka ya Mapato nchini (TRA), Bw. Richard Kayombo, aliwasilisha mada juu ya umuhimu wa kuingiza masuala juu ya elimu ya kodi katika mitaala ya Elimu ngazi ya Msingi na Sekondari.

"TRA inaamini kwamba kama kungekua na somo la kodi linalosomwa na wanafunzi wote katika shule za Msingi na Sekondari tungeweza kuwa na raia wanaoelewa kodi" alisema Bwana Kayombo.

Aidha amesema, TRA inakusanya kodi kutoka kwa walipa kodi ambao hawana ufahamu na hawajui umuhimu wa kulipa kodi hivyo kama wanafunzi watafundishwa somo la kodi shuleni, itasaidia kupata raia wenye uelewa mpana kuhusu kodi na kujenga utamaduni wa kulipa kodi kwa hiyari.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa kamati Prof.Maboko aliwashukuru TRA kwa maoni na mapendekezo waliyoyatoa na kuahidi kuyafanyia kazi katika maboresho ya Mtaala wa Elimu nchini yanayoendelea.

WAKUFUNZI WA VYUO VYA UALIMU WATOA MAONI YA MTAALA WA UALIMU

Na. Mwandishi Wetu – Morogoro.

Kamati ya Kitaifa ya Uboreshaji Mitaala iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof Adolf Mkenda pamoja na Wakuza Mitaala wa Taaasisi ya Elimu Tanzania (TET) wamepata nafasi ya kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa Wakufunzi wa Vyuo Ualimu Kanda ya Mashariki kuhusiana na mapendekezo ya maboresho ya Mitaala ya Elimu ya Ualimu.

Katika kikao hicho kilichofanyika Mjini Morogoro, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Prof. Makenya Maboko aliwasilisha mapendekezo ya muundo wa elimu ya ualimu na mabadiliko ya mtaala yanayopendekezwa ambapo amesema kuwa, wakufunzi hao wana nafasi ya kutoa maoni yao kwa kamati na itayapokea na kuyafanyia kazi.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa TET Dkt. Aneth Komba amewashukuru wakufunzi hao kwa muda wao wa kushiriki kwenye utoaji wa maoni huku akiwasilisha wasilisho juu ya matokeo muhimu kutoka kwenye taarifa ya uchambuzi wa maoni ya wadau kuhusu elimu ya ualimu.

Dkt. Komba ameeleza kuwa maboresho ya mitaala yanayofanyika niya sita tangu nchi ipate uhuru na ameeleza kuwa maboresho hayo ni makubwa yenye lengo la kutekeleza azma ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuwa na wahitimu wenye ujuzi wa kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya siku kwa siku.

WAZIRI MKENDA APIGIA CHAPUO MAFUNZO YANAYOTOLEWA NA ADEM

Na. Mwandishi Wetu – Bagamoyo.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof. Adolf Mkenda ameunga mkono na kuipongeza ADEM kwa utoaji wa mafunzo ya Uongozi, Usimamizi na Uthibiti Ubora wa Elimu yanayojenga umahiri kwa walimu, na wadau wengine wa elimu katika nyanja ya Uongozi, Usimamizi na Uthibiti Ubora wa Elimu nchini.

Prof. Mkenda ameyasema hayo novemba, 25, 2022 katika hotuba yake iliyosomwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Sera na Tafiti kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Ladislaus Mnyone aliyemwakilisha Mhe Waziri Mkenda katika Mahafali ya 30 ya ADEM yaliyofanyika ADEM Bagamoyo.

Akizungumza na wahitimu katika mahafali hayo kwa niaba ya Waziri Mkenda, Prof. Mnyone amesema ADEM imejizatiti na inafanya kazi nzuri katika kuboresha mazingira ya utoaji mafunzo ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu pamoja na Uthibiti Ubora wa Shule hivyo Walimu waliohitimu mafunzo hayo wamepikwa na kuiva katika eneo la Uongozi, Usimamizi na Uthibiti Ubora wa Elimu.

"Ninaipongeza ADEM kwa kuendesha kozi mbalimbali zikiwemo za Astashahada na Stashahada na ubunifu wa uandaaji wa Mtaala wa Shahada ya Usimamizi wa Uthibiti Ubora wa Elimu ili kuendana na mabadiliko ya kisekta na kuimarisha utendaji kazi katika ngazi mbalimbali za elimu" Amesema Prof Mnyone

Ameongeza, ninaielekeza Menejimenti ya ADEM, kuendelea kuboresha mafunzo ya Muda Mfupi na Muda Mrefu, kwa kuzingatia mahitaji ya soko na mabadiliko mbalimbali yanayotokea katika sekta ya elimu huku akitanabaisha kuwa Wizara itaendelea kufanya uboreshaji wa miundombinu ya ujifunzaji na kufundishia kwa kutoa rasilimali fedha na ushauri ili kuhakikisha inakijengea Chuo uwezo zaidi wa kutoa mafunzo.

Nae Mtendaji Mkuu wa ADEM, Dkt. Siston Masanja Mgullah akizungumza katika Mahafali hayo amesema jumla ya Walimu 869 wamehitimu mafunzo yao ambapo Wahitimu 699 ni wa Stashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu (DEMA), wahitimu 169 ni wa Stashahada ya Uthibiti Ubora wa Shule na

WAZIRI MKENDA APIGIA CHAPUO MAFUNZO YANAYOTOLEWA NA ADEM

Mhitimu mmoja amehitimu mafunzo ya Astashahada ya Uongozi, Usimamizi na Utawala wa Elimu (CELMA).

"Ni mategemeo yetu ni kuwa, wahitimu wa kozi ya Uongozi na Usimamizi wa elimu kwa ngazi za Astashahada na Stashahada wataongoza vizuri shule, kupanga mipango inayotekelezeka, kusimamia utekelezaji wa mtaala pamoja na upimaji wa maendeleo ya wanafunzi kwa umahiri" Amesema Dkt Masanja.

Ameongeza kuwa, wahitimu wa kozi ya Uthibiti Ubora wa Shule wana uwezo wa kuunda timu za uthibiti ubora wa shule, kuandaa vigezo vya shule fanisi na kufanya ufuatiliaji wa karibu wa shughuli za shule ikiwemo ufundishaji na ujifunzaji na kuzisaidia shule kuimarisha tahadhari dhidi ya majanga kama vile moto ili kupunguza athari za zake shuleni.

Bw. Emmanuel Qeresh mmoja wa wahitimu wa mafunzo ya ADEM katika Mahafali ya 30 ya ADEM akizungumza kwa niaba ya Wahitimu wenzake amesema, Mafunzo waliyoyapata ADEM yatawasaidia sana kuwa Viongozi, wasimamizi na wathibiti Ubora wa Elimu mahiri katika Shule wanazosimamia.

Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM) unafanya shughuli zake chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ukiendesha mafunzo ya Muda Mrefu na Muda Mfupi ya Uongozi, Usimamizi na Uthibiti Ubora wa Elimu, lengo likiwa ni kuboresha Uongozi na Usimamizi wa elimu nchini katika shule za Msingi, Sekondari, Vyuo vya Ualimu na kwa Maafisa Elimu wote kuanzia ngazi ya Kata, Wilaya, Mkoa na Taifa.

PROF. MKENDA ASEMA TUKO TAYARI KWA MJADALA WA KITAIFA KUHUSU MAPENDEKEZO YA SERA YA ELIMU NA MITAALA

Na. Mwandishi Wetu – Mwanza.

Mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na Mitaala ya Elimu Msingi yamekamilika na yanasubiri mchakato wa ndani ya Serikali ili kupata ridhaa ya rasimu zilizoandaliwa kupelekwa kwa wadau kwa mjadala wa kitaifa.

Hayo yameelezwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Profesa Adolf Mkenda, wakati akizungumza katika Mahafali ya 41 ya Chuo Kikuu Huria (OUT) Jijini Mwanza, ambapo amesema kuna mambo makubwa ambayo yamependekezwa na wadau mbalimbali.

Prof. Mkenda amefafanua kuwa utekelezaji wa kazi hiyo umeendelea kwa kushirikisha wadau mbalimbali wakiwemo Maaskofu, Mashekhe, Walimu, wenye Shule Binafsi pamoja na wataalamu kutoka nje ya nchi ili kupata uzoefu kutoka katika nchi zilizoleta mageuzi ya elimu na kufanikiwa na zile ambazo hazikufanikiwa.

"Tumekamilisha rasimu ya mapitio ya Sera, ina mapendekezo mengi makubwa, tunachosubiri sasa ni mchakato wa ndani wa kupitia mapendekezo hayo kabla hatujayatangaza rasmi kwa ajili ya mdahalo wa Kitaifa na hatimae mchakato wa maamuzi uweze kufikiwa ndani ya Serikali," amesema Prof. Mkenda.

Akitolea mfano jambo moja ambalo limeguswa katika mapitio ya Sera hiyo amesema ni pamoja na suala la Walimu kupewa kipaumbele katika ubora na suala la mafunzo endelevu kazini ambalo hata sasa suala hilo la mafunzo kazini limeshaanza na linaendelea.

"Katika mapitio ya Sera, Walimu waliopo wataendelea kupewa mafunzo kazini, ambayo tayari wameshaanza kuyapata na Walimu wapya tutaona vigezo katika mapitio ya Sera kuhakikisha tunakuwa na Walimu bora wa kuendeleza elimu yetu," amefafanua Prof. Mkenda.

Aliongeza kuwa kazi ya kupitia mitaala nayo inakwenda vizuri pamoja na kuwa kwa kawaida hapa nchini kazi hiyo ilikuwa hailepelekwi katika ngazi ya maamuzi kutokana na kuwa ni kazi ya kitaalamu zaidi, lakini kwa mageuzi haya ya elimu italetwa kwenye ngazi za juu na kisha kujadiliwa na Umma wa Watanzania.

Ameongeza kuwa mageuzi hayo ya mitaala yatafanyika pia katika ngazi ya Elimu ya Juu ambapo huko utaangaliwa zaidi ubora wa elimu.

WALIMU 265 WAPANDISHWA VYEO, 67 WASTAAFU MULEBA

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Muleba mkoani Kagera imewapandisha vyeo walimu 265 wa shule za msingi na sekondari huku walimu 56 wakistaafu kazi katika mwaka wa fedha 2021/2022 na 39 wakistaafu katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/2023.

Hayo yamebainika katika taarifa ya timu ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu ya TSC ngazi ya wilaya iliyofanya ziara katika ofisi ya TSC Muleba hivi karibuni kwa lengo la kuona namna ofisi hiyo inavyotoa huduma kwa walimu.

Tume ilieleza "katika zoezi la upandishwaji vyeo walimu vigezo vyote huzingatiwa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha uwepo Ikama na Bajeti iliyoidhinishwa, Taarifa za utendaji kazi za Walimu (OPRAS, Muundo wa kada ya Walimu, Kisahihisho "A" Miundo ya kada ya Walimu, Waraka wa Mwaka 2014 na Tange iliyohuishwa," ilieleza sehemu ya taarifa hiyo.

Pamoja na idadi hiyo ya walimu waliopandishwa vyeo, taarifa ilieleza kuwa kuna walimu 12 ambao walikuwa na sifa lakini hawakupandishwa kwa sababu mbalimbali lakini waliombewa kibali kufuatia maelekezo ya Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuwataka waajiri kuawasilisha orodha ya watumishi ambao walikuwa na sifa lakini hawakupandishwa vyeo.

"TSC kwa kushirikiana na ofisi ya mwajiri zinaendelea kufuatilia kwa karibu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili vibali vya walimu 12 ambao hawakupandishwa vyeo viweze kupatikana na walimu hao wapandishwe," ilieleza sehemu ya taarifa hiyo.

Kwa upande wa hitimisho la kazi ya ualimu, taarifa hiyo ilieleza kuwa TSC muleba ilitoa vibali vya kustaafu kazi kwa walimu 67 ambapo katika mwaka 2021/2022 jumla ya vibali 28 vya kustaafu vilitolewa ambapo walimu tisa (9) walistaafu kwa lazima na walimu 19 walistaafu kwa hiari.

"Katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/2023 walimu 39 walistaafu ambapo 11 walistaafu kwa lazima na 28 walistaafu kwa hiari na hakuna mwalimu aliyestaafu kwa ugonjwa," ilisema taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilielezea kuhusu mafunzo ya walimu na kuthibitisha uwepo wa Mpango wa Mafunzo ulioandaliwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa na kufafanua kuwa Mpango huo unazingatia utoaji ruhusa za masomo kwa walimu ambapo walimu 206 wako masomoni kwa mwaka 2021/2022.

Kwa upande wa nidhamu, taarifa ilieleza kuwa katika mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya mashauri 19 yalipokelewa na yote yalihitimishwa huku ikithibitisha kuwa sheria, kanuni na taratibu zilizingatiwa katika kushughulikia mashauri hayo.

"Timu ilipitia na kukagua kuona kama Sheria, Kanuni na Taratibu zinazingatiwa katika uendeshaji wa Mashauri ya Nidhamu, na kubaini kuwa Kanuni ya 15, 16, 17, 18, 19 na 20 ya Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu za mwaka 2016 zinazingatiwa kwenye maeneo yafuatayo; Namna ya uendeshaji wa Uchuguzi wa awali unavyofanyika, Kamati ya Nidhamu kuridhia kuanzishwa kwa Shtaka; Usahihi wa Uandishi wa Hati za Mashtaka; Kuandikwa Kanuni iliyokiukwa kwa usahihi na Kosa kuwa miongoni mwa makosa yaliyoorodheshwa kwenye Kanuni," ilieleza.

Tarifa hiyo iliendelea kufafanua mambo yaliyozingatiwa kwenye kanuni hiyo kuwa "Maelezo ya shtaka yametaja muda, mahali na namna kosa lilivyofanyika; kosa ni mahususi au la ujumla; Hati ya Mashtaka imetumika na siyo barua; Hati ya Mashtaka ina jina na saini ya Katibu wa Kamati na siyo Kaimu Katibu au kwa niaba (kny); Hati za Mashtaka zilizorekebishwa au kufutwa ndani ya siku 30 tangu kutolewa ambapo (Hati mpya ni lazima ioneshe kufutwa au kurekebishwa kwa Hati ya awali)".

Pamoja na hayo, "Timu ilipitia na kuona ushahidi wa kutumwa Hati ya Mashtaka (Rejesta ya posta na Dispatch), uzingatiaji wa sifa katika uteuzi wa Kamati ya Uchunguzi; Usahihi katika Uandaaji wa Hadidu za Rejea; Uwepo wa barua za Wito kwenye uchunguzi; Ushahidi namna mtuhumiwa alivyotumiwa barua ya wito; Uwepo wa taarifa ya

WALIMU 265 WAPANDISHWA VYEO, 67 WASTAAFU MULEBA

Kamati ya uchunguzi, adhabu zilitolewa kuzingatia Kanuni tu na ziwe zimeandikwa kwa usahihi, adhabu kuzingatia mwenendo wa shauri na uzito wa kosa lililothibitika pamoja na uwepo wa uthibitisho wa kutuma barua za uamuzi kwa wahusika," ilifafanua.

Wilaya ya Muleba ni moja ya Wilaya saba katika mkoa wa Kagera, wilaya hii ina tarafa tano (5), Kata 43, Vijiji 166 na Vitongoji 677. Wilaya ina shule za msingi 233 za serikali na za Binafsi 17, shule za Sekondari za Seikali zipo 51 na za binafsi 16 na chuo cha Ualimu kimoja (1) .Wilaya ya Muleba ina Jumla ya walimu 3037 ikiwa ni pamoja na walimu 2286 wa Elimu Msingi (wakiume 1367 na wakike 919) na walimu wa Sekondari 751 (wakiume 563 na wakike 188).

OFISI ZA TSC WILAYA ZASHAURIWA KUWA NA MKAKATI KUWAJENGEA UWEZO WAKUU WA SHULE

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi ya Wilaya zimeshauriwa kuweka mkakati wa kuwajengea uwezo Wakuu wa Shule ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi kwa kuwa ndio mamlaka ya kwanza ya nidhamu kwa walimu.

Ushauri huo umetolewa na timu ya ufuatiliaji wa majukumu ya TSC ngazi ya wilaya iliyofanya ziara katika ofisi za TSC za Kilindi, Tanga Jiji, Pangani na Mkinga hivi karibuni ambapo ilibaini kuwa ofisi za wilaya bado hazina mkakati madhubuti wa kuwajengea uwezo viongozi hao wa shule.

Taarifa iliyotolewa na timu hiyo ilieleza kuwa lengo la ufuatiliaji lilikuwa ni kuona namna majukumu ya Tume katika ngazi ya Wilaya yanavyotekelezwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu, Miongozo na maelekezo/maagizo yanayotolewa na Tume/Serikali, kufanya tathmini ya ufanisi uliotokana na mafunzo yaliyotolewa kwa Watumishi wa Tume na Wajumbe wa Kamati za Wilaya pamoja na kubaini changamoto za kiutendaji zinazowakabili watendaji wa Tume ngazi ya Wilaya ili ziweze kufanyiwa kazi na hatimaye kupatiwa ufumbuzi.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa, Wakuu wa Shule wana wajibu mkubwa wa kuwasaidia walimu wanaowasimamia ili watekeleze majukumu yao kwa kuzingatia miiko na maadili ya kazi ya ualimu, hivyo kuwajengea uwezo ni jambo lisiloepukika.

"Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015 inawatambua wakuu wa shule kama mamlaka ya kwanza ya nidhamu kwa walimu. Changamoto iliyopo ni kwamba Ofisi za Wilaya bado hazijaweka mpango mkakati wa namna ya kuwafikia viongozi hao na kuwajengea uwezo katika utekelezaji wa majukumu yanayohusu utumishi wa walimu," ilieleza sehemu ya taarifa hiyo.

Ilifafanua kuwa, baadhi ya Wakuu wa Shule wanashindwa kutekeleza majukumu yao hususan pale wanapohitajika kuchukua hatua za kinidhamu na kuendesha mashauri ya walimu wanaokiuka taratibu na badala yake mashauri hayo yanapelekwa ngazi ya wilaya kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Miongoni mwa sababu za wakuu wa shule kushindwa kuchukua hatua za nidhamu kwa walimu ni kutoelewa kwa undani sheria, kanuni na taratibu za masuala ya kiutumishi, kuogopa lawama kwa walimu wanaowasimamia na wakati mwingine kushiriki vitendo vya ukiukaji wa maadili ya kazi ya ualimu.

"Moja ya suluhisho la sababu za walimu kushindwa kuchukua hatua ni kuwajengea uwezo ili waweze kuzielewa taratibu za kiutumishi lakini pia kuwapa elimu ya kujiamini na kusimamia sheria bila kujali lawama pamoja na kuwaelimisha kuwa wanapaswa kuwa mfano wa kuigwa na walimu wengine kwa kuwa na tabia njema kwa kuwa wao ni viongozi," ilieleza taarifa hiyo.

Pamoja na hilo, taarifa hiyo ilishauri kwamba walimu wa ajira mpya wasimamiwe kwa ukaribu zaidi wakati wa kujaza taarifa za kiutumishi hususan anuani zao ili hata pale wanapokuwa nje ya vituo vya kazi iwe rahisi kufanya mawasiliano rasmi.

"Baadhi ya walimu hawakuweka last known address kwenye history sheet zao jambo linalofanya iwe vigumu kuwatumia nyaraka wakati wa mashauri ya nidhamu iwapo hawapo vituoni," ilisema tarifa hiyo.

Kuhusu kuzingatia taratibu katika kushughulikia mashauri ya nidhamu, taarifa hiyo ilieleza kuwa ni muhimu kwenye jalada la mhusika kuonekane ushahidi wa kimaandishi wa kufanyika kwa uchunguzi wa awali kabla ya kuanzisha shauri, kuwepo na ushahidi wa mtuhumiwa kutumiwa Hati ya Mashtaka, Barua ya Wito kuhudhuria kwenye Kamati ya Uchunguzi na Barua ya Uamuzi.

TATHMINI YA IDADI NA HALI YA MIUNDOMBINU KATIKA SHULE ZA MSINGI MKOANI IRINGA IMEONYESHA KUENDELEA KUIMARIKA

- Mazingira ya utendaji kazi kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari nchini yaendelea kuimarishwa;
- Shule 43 Mkoani Iringa zafikiwa kwa tathmini ya idadi na miundombinu:
- Yabainika hakuna madai ya upandaji madaraja kwa Walimu kama sehemu ya kupata haki, maslahi na stahiki za kiutumishi;
- Ushiriki wa wananchi kwenye miradi ya maendeleo inayotekelezwa shuleni kwa fedha za Serikali wapongezwa;

  Wahandisi wa Sekretarieti za Mikoa na Serikali za Mitaa wasisitizwa kutembelea miundombinu ya shule katika maeneo yao;
- TARURA yashauriwa kujenga na kuimarisha vivuko ili vipitike kwa nyakati zote kudumisha na kuimarisha mahudhurio ya wanafunzi katika masomo shuleni; na
- Yabainika Wananchi wanaoishi mijini kutokuwa na mwamko wa uchangiaji katika miradi ya maendeleo ya elimu kutokana na mwingiliano mkubwa wa siasa.

Na. Mwandishi Wetu - Dodoma.

Serikali kupitia miradi ya Sekta ya Elimu imeendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari nchini ikienda pamoja na uimarishaji wa miundo mbinu ya Shule, ujenzi wa madarasa kuanzia Awali kwa kutoa kipaumbele zaidi kwenye shule zenye wanafunzi wengi zaidi.

Hilo limeonekana katika taarifa ya uhakiki wa tathmini ya idadi na hali ya miundombinu katika Shule za Msingi kupitia Mradi wa BOOST mkoani Iringa wenye jumla ya Halmashauri Tano; Manispaa ya Iringa, Wilaya ya Iringa, Kilolo, Mufindi na Mji wa Mafinga ambapo jumla ya shule 43 zilifikiwa kwa tathmini.

Taarifa hiyo imesema pamoja na mambo mengine ya kufuatilia haki na maslahi ya Walimu kiutumishi katika vituo vyao vya kazi, sehemu ya malengo ya ufuatiliaji huo yalikuwa ni pamoja na kuhakiki hali ya miundombinu ya Shule za Msingi, kuthibitisha shule zenye uchakavu, hali ya msongamano wa wanafunzi, kuthibitisha hali ya shule zisizo na miundombinu ya kudumu, kubaini maeneo yanayopendekezwa kujengwa shule mpya, kubaini shule ambazo wanafunzi wanapita katika maeneo hatarishi ili kufika shuleni, kubaini vijiji/mitaa ambayo haina shule za msingi, kufuatilia hali ya ujenzi wa madarasa ya shule za sekondari chini ya mradi wa madarasa 8,000 ya Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na kujiridhisha eneo la mapokezi ya vifaa vya maabara chini ya mradi wa EP4R kwa kuzingatia taratibu zilizopo.

Matokeo ya tathmini ya uhakiki huo yameonyesha kuiridhisha timu ya ufuatiliaji katika wilaya hizo mkoani Iringa kwa asilimia 95 ambapo asilimia tano iliyobaki ilitokana na kuanzishwa kwa vituo shikizi ambavyo vilipata usajili siku za karibuni na hivyo kutokuwa vimeingizwa kwenye mfumo na baadhi ya shule kutofautiana kwenye taarifa zilizowasilishwa.

Taarifa hiyo imepongeza

TATHMINI YA IDADI NA HALI YA MIUNDOMBINU KATIKA SHULE ZA MSINGI MKOANI IRINGA IMEONYESHA KUENDELEA KUIMARIKA

ushiriki wa wananchi kwenye miradi ya maendeleo inayotekelezwa shuleni kwa fedha za Serikali huku ikibainisha baadhi ya maoni na mapendekezo ya timu katika kila ngazi iliyotembelewa kuwa ni Pamoja; kutathmini mchango wa wananchi ili kujua gharama halisi iliyotumika, Wahandisi kuendelea kutoa ushauri wa kitaalamu baada ya kufanya tathimini ya miundombinu ya shule, Mikoa kuwa na mipango ya kukusanya taarifa sahihi za miundombinu ya shule katika maeneo yao, Halmashauri kupima maeneo ya shule na kusaidia kupatikana kwa hati miliki, Idara za Elimu kuzishirikisha idara nyingine katika kutatua changamoto za miundombinu ya shule, mikakati ya kuwapatia wanafunzi wote chakula shuleni iwekwe na kutekelezwa, kuishauri TARURA kujenga na kuimarisha vivuko ili vipitike kwa nyakati zote kwani baadhi ya sehemu kuna changamoto ya wanafunzi kuvuka mabonde wakati wa mvua kwa sababu ya kukosekana vivuko na hivyo kufifisha mahudhurio ya masomo darasani kwa baadhi ya misimu.

Vilevile taarifa hiyo ilishauri kutumia wadau mbalimbali wenye ari ya kusaidiana na jamii katika kuleta maendeleo ya shule hapa nchini ikiambatana na motisha kwa wananchi kuwapongeza kwa njia mbalimbali ikiwamo kutoa vyeti ngazi ya kijiji na mitaa inayoshiriki katika maendeleo ya elimu, kuwepo kwa mawasiliano na ushirikiano dhabiti kati ya shule na shule na shule na halmashauri na maeneo ya mijini kujenga nyumba za kwenda juu (magorofa) kutokana na ukosefu wa maeneo.

Katika kuainisha yaliyojitokeza wakati wa zoezi la ufuatiliaji, taarifa hiyo ya timu ya wataalam ilisema kuwa sehemu kubwa ya wananchi wameonekana kuwa na mwitikio mkubwa katika shughuli za maendeleo ya elimu hapa nchini hususan wanaposhirikishwa kwenye mipango ya shule wakijitoa kwa nguvu na mali huku wananchi wa maeneo ya mijini hasa wanaoishi kwenye Manispaa wakibainika kutokua na mwamko mkubwa wa uchangiaji kutokana na mwingiliano mkubwa wa kisiasa.

Aidha, mmoja wa wataalam katika timu hiyo ambaye pia ni Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Mbena Nkwama, *ndc*; akiongea na mwandishi wetu ofisini kwake alisema katika shule zote 43 zilizotembelewa na kufanyiwa tathmini ndani ya Halmashauri Tano (Manispaa ya Iringa, Wilaya ya Iringa, Kilolo, Mufindi na Mji wa Mafinga) Mkoani Iringa, walimu waliohojiwa walithibitisha kupandishwa cheo, hakuna hata mmoja anayedai daraja. Hii ni juhudi kubwa iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan , Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kushughulikia na kuondoa kabisa madai ya walimu pamoja na kuwaimarishia mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi.

Alisema kwa jitihada hizo za Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan, katika kuhakikisha Walimu wanatekeleza wajibu wao bila vikwazo kilichobaki ni Serikali kuwadai uwajibikaji wao kwani Serikali imeshatimiza na inaendelea kutimiza mahitaji yao.

Katibu huyo aliendelea kuwasisitiza Walimu nchini kutii na kufuata Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo yote ya Utumishi wa Umma na Nguzo Kuu za Ualimu huku akielekeza

TATHMINI YA IDADI NA HALI YA MIUNDOMBINU KATIKA SHULE ZA MSINGI MKOANI IRINGA IMEONYESHA KUENDELEA KUIMARIKA

Ofisi za TSC Wilayani kuongeza jitihada katika kutoa elimu hiyo baada ya timu kubaini asilimia kadhaa ya Walimu wa ajira mpya kutokuwa na uelewa hasa katika kufuatilia stahili zao za msingi za kiutumishi kama kupewa barua na mikataba yao ya ajira, pamoja na kuthibitishwa kazini kwa wakati unaostahili.

Huu ni mwendelezo wa jitihada za Serikali katika kufanya maandalizi ya kuwapokea wanafunzi wa Kidato cha Kwanza mwakani 2023 ikizingatiwa siku za hivi karibuni Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia lilitoa taarifa ya matokeo ya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi (PSLE) ambapo Kaimu Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, Athumani S. Amasi, katika Mkutano wake wa 148 uliofanyika tarehe 28/11/2022 alisema Baraza liliidhinisha kutangazwa kwa matokeo ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi uliofanyika kuanzia tarehe 05 hadi 06 Oktoba, 2022 huku matokeo hayo yakiainisha kusajiliwa kwa jumla ya watahiniwa 1,384,186 wa Shule za Msingi kufanya mtihani huo wakiwemo Wasichana 723,027 sawa na asilimia 52.23 na Wavulana 661,159 sawa na asilimia 47.77 huku kati ya watahiniwa hao waliosajiliwa, watahiniwa wenye mahitaji maalum wakiwa 4,221 sawa na asilimia 0.30.

Kaimu Katibu Mtendaji huyo wa Baraza alisema Watahiniwa 1,350,881 sawa na asilimia 97.59 ya waliosajiliwa walifanya mtihani huku kati yao wakiwa ni Wasichana 709,556 sawa na asilimia 98.14 na Wavulana walikuwa 641,325 sawa na asilimia 97.00 akisema watahiniwa 33,305 sawa na asilimia 2.41 hawakufanya mtihani kutokana na sababu mbalimbali, zikiwemo utoro na ugonjwa. Kati yao Wasichana ni 13,471 na Wavulana ni 19,834.

Ndg. Amasi akifafanua eneo la ufaulu wa ujumla alisema jumla ya watahiniwa 1,073,402 kati ya 1,348,073 wenye matokeo ambao ni sawa na asilimia 79.62 wamefaulu ambapo wamepata Madaraja ya A, B na C akichanganua ufaulu huo kuwa kati yao ni Wasichana 558,825 ambao ni sawa na asilimia 78.91 na Wavulana ni 514,577 sawa na asilimia 80.41.

Katika matokeo ya mtihani huo kwa mwaka 2021 ; Watahiniwa waliofaulu walikuwa 907,802 sawa na asilimia 81.97. Hivyo, kitakwimu kuna punguo la ufaulu kwa asilimia 2.35 japokuwa idadi ya watahiniwa waliofaulu imeongezeka kwa watahiniwa 165,600 sawa na asilimia 18.24 ikilinganishwa na mwaka 2021.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 **Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz** **Tovuti: www.tsc.go.tz**

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania